

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**BUNGE LA KUMI NA MBILI**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KWANZA**

**Kikao cha Pili – Tarehe 11 Novemba, 2020**

*(Bunge Lillianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaweza kukaa.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea ningeomba kuwataarifu kwamba kwenye Mkutano wa Kwanza wa Bunge jipya kama huu wa kwetu huwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano anahutubia Bunge kwa maana ya kuweka dira ya Serikali yake kwa miaka mitano inayokuja na utekelezaji wa Ilani kadri anavyoona inafaa. Hotuba hiyo ni muhimu, anahutubia Bunge, lakini kupitia Wabunge anakuwa analihutubia Taifa.

Kwa hiyo, naomba niwataharifuni kwamba kesho kutwa, siku ya Ijumaa saa tatu kamili asubuhi tutaomba Waheshimiwa Wabunge wote tuwe ndani ya Ukumbi huu na maelekezo mengine tutayapata siku hiyo au kesho, tutaanza na gwaride hapo nje na utaratibu mwingine, pia tutakuwa na wageni kwenye *galleries* zetu, tutaomba sana uwahi kufika. Nikisema saa tatu kamili uwe umekaa kwenye kiti maana yake tuanze kuwasili saa mbili kamili, vinginevyo barabara huko nje unaweza ukawa kwenye barabara ambayo huwezi kukatiza siku hiyo.

Kwa hiyo ni vizuri sana tukawahi na kila mmoja wetu akawepo na Mheshimiwa Mbunge yeyote yule ambaye ametoka kwenda popote pale basi natoa wito turudi Dodoma tayari kuisikiliza hotuba hiyo wenyewe, tuweze kumpokea Rais wetu, tumpe kila aina ya ushirikiano. Wale mliokuwa mnafikiria kuondoka basi msiondoke kwanza ili zoezi hilo liweze kwenda kwa salama na amani. Narudia tena saa tatu kamili kesho kutwa Ijumaa tuwe *seated* hapa na taratibu nyingine zitaendelea kama ilivyo ada.

Katibu kwa shughuli za leo.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

**KIAPO CHA UAMINIFU KWA WABUNGE**

*(Kiapo cha Uaminifu Kinaendelea)*

**SPIKA:** Kiapo cha uaminifu. Tunaendelea.

**NDG. PAMELA E. PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

305. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi
306. Mhe. Eric James Shigongo
307. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde
308. Mhe. Luhaga Joelson Mpina
309. Mhe. Mariam Omary Ukiwaona Ramadhani Ditopile  
Mzuzuri Mwinshehe
310. Mhe. Martha Nehemia Gwau
311. Mhe. Miraji Jumanne Mkonongo Mtaturu
312. Mhe. Zahoro Mohamed Haji
313. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka
314. Mhe. Regina Ndege Qwaray
315. Mhe. Samweli Xaday Hhayuma
316. Mhe. Shally Josepha Raymond
317. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo
318. Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula
319. Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya
320. Mhe. Sylvia Francis Sigula
321. Mhe. Taska Restituta Mbogo

322. Mhe. Tauhida Cassian Gallos
323. Mhe. Tecla Mohamed Ungele
324. Mhe. Umy Hamisi Nderiananga
325. Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo
326. Mhe. Vita Rashid Kawawa
327. Mhe. William Tate Olenasha
328. Mhe. Yahaya Omary Massare
329. Mhe. Zacharia Paulo Issaay
330. Mhe. Zainab Athuman Katimba
331. Mhe. Zaytun Seif Swai
332. Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka
333. Mhe. Zuweni Athuman Bushiri
334. Mhe. Anne Kilango Malecela
335. Mhe. Cosato David Chumi
336. Mhe. Pauline Philipo Gekul
337. Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda
338. Mhe. January Yusuf Makamba
339. Mhe. Nape Moses Nnauye
340. Mhe. Rehema Juma Migilla
341. Mhe. Neema Kichiki Lugangira
342. Mhe. Toufiq Salim Turkey
343. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba
344. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi
345. Mhe. Amandus Julius Chinguile
346. Mhe. Aysharose Ndogholi Mattembe
347. Mhe. George Boniface Simbachawene
348. Mhe. Omari Juma Kipanga
349. Mhe. Dkt. Ritta Enespher Kabati
350. Mhe. Neema William Mgaya
351. Mhe. Stella Ikupa Alex
352. Mhe. Umy Ali Mwalimu
353. Mhe. Salma Rashid Kikwete
354. Mhe. Lucy Thomas Mayenga

*(Wabunge Waliotajwa Hapo Juu Waliapa Kiapo  
cha Uaminifu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naendelea kuisitiza kuhusu umuhimu wa kurudisha hizi karatasi zetu za njano ambazo tunapewa kuzisaini, ni muhimu sana. Kama

nilivyowaeleza jana zitatusaidia sana katika masuala ya kiutawala na Waheshimiwa Wabunge najua mmewasili siku kadhaa sasa, lakini baada tu ya kuapa hapa sasa mambo yote tutarekebisha yanayohusiana na utaratibu. *(Makofi)*

Pia natambua kwamba Waheshimiwa Wabunge mnao wageni wengi, mnayo mambo mengi ya kurekebisha hapa mjini, wengine bado mambo ya makazi hayajakaa sawasawa, wengine simu za wajumbe bado nyingi sana, Mzee umeshafika Dodoma? *(Kicheko)*

Wajumbe bado wanawafuatilia kwa hiyo, lazima mpate muda wa kuwasiliana na wajumbe huko na wengine wamekuja. Wabunge ni watu wenye shughuli nyingi sana. Kwa hiyo, tumeona mchana wa leo tuwaachie muwe huru mrekebishe mambo yenu ili tuweze kukutana kesho Saa Tatu kwa shughuli muhimu za kesho pia. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi hiyo basi, naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 3.45 Asubuhi, Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 12 Novemba, 2020 Saa 3.00 Asubuhi)*